# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

# OFISI YA WAZIRI MKUU

# TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

# HALMASHAURI YA MJI WA MBULU

# SHULE YA SEKONDARI KAINAM

# MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI KAINAM

**SHULE YA SEKONDARI KAINAM**

**S.L.P 158**

**MBULU**

**TAREHE ……………………**

**FOMU YA MAELEKEZO YA KUJIUNGA KIDATO CHA TANO MWAKA JULAI 2026**

**MAWASILIANO**

0621-556407/0782625696 – MKUU WA SHULE

**0786156154/0623994395** – MAKAMU MKUU WA SHULE

MZAZI/MLEZI WA ______________________________________

TAHASUSI ________________ KIDATO CHA TANO MWAKA…………

S.L.P ___________

**YAH: <u>KUCHAGULIWA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI KAINAM KIDATO CHA TANO (V) MWAKA…………</u>**

1. **<u>UTANGULIZI</u>**

Kwa namna ya pekee kabisa napenda kukujulisha kuwa umechaguliwa kujiunga kidato cha tano katika shule ya sekondari Kainam kwa mwaka wa masomo julai…………

Shule ya sekondari Kainam ni shule ya bweni kwa wanafunzi wa kidato cha tano na sita, kwa mwaka huu wa…….., shule hii ina tahasusi EGM,HGK, HKL, HGLi na HGFa. Shule ni ya wavulana na wasichana

Muhula wa masomo utaanza tarehe ………………… hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni tarehe………………….. Na mwisho wa kuripoti ni tarehe………………………..

2. **MAHALI SHULE ILIPO**

Shule ya sekondari Kainam ipo katika mkoa wa Manyara, Halmashauri ya Mbulu Mji. Shule ipo umbali wa kilometa 12 kutoka

makao makuu ya halmashauri ya Mbulu mji. Ili uweze kufika Kainam sekondari kwa urahisi fuata maelekezo yafuatayo.

- **KWA WATAKAOANZIA SAFARI ARUSHA AU KUPITIA ARUSHA PANDA MAGARI (KRUZA ZA MBULU)**
- **KWA WATAKAOANZIA SAFARI AU KUPITIA NJIA YA DODOMA AU SINGIDA SHUKIA STENDI KUU YA MABASI YA BABATI KISHA PANDA MAGARI (KRUZA ZA MBULU)**
- **KWA WATAKAOPITIA NJIA YA HYDOM AU KARATU PANDA MAGARI YA MBULU.**

Utakapofika stendi ya Mbulu ulizia stendi ya haysi na bodaboda za Kainam, usafiri kutoka Mbulu hadi Kainam sekondari ni Tsh 6000/=

# Nakutakia safari njema

## Karibu sana shule ya sekondari kainam

## 3. MAMBO MUHIMU YA KUFANYA NA KUZINGATIA

Pamoja na kukupongeza kwa kufanikiwa kupata nafasi hii muhimu ya kujiunga na kidato cha tano, ninatumia fursa hii kusisitiza yafuatayo;-

a) Kusoma kwa makini: maelezo yote katika fomu hii ya kujiunga (joining instructions) kidato cha tano shule ya sekondari kainam ili kuyatekeleza bila kisingizio na utekelezaji wake, utaleta ufanisi na tija katika kupata elimu iliyobora kwa muda wote na masomo yako hapa shuleni
b) Kuzisoma na kuzielewa sheria za shule ndiyo msingi wa uendeshaji wa shule
c) Kujaza fomu No 1&2 na kuzirudisha shuleni siku ya kuripoti utakapofika
d) Utakapofika kwenye shule hii utatakiwa kusoma kwa bidii sana na kufaulu mitihani yote ili kufanikisha malengo yako.

## 4. MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA (WASICHANA)

**a) SARE ZA SHULE**

- Sketi mbili (2) rangi ya draft (grade one), rinda box, zipu ikiwa pembeni kushoto na mfuko wa kulia. Urefu wa sketi uguse kifundo cha mguu (mwanafunzi mwenye sketi fupi hatapokelewa.
- mashati meupe mawili tetron mikono mirefu
- Tai 2 rangi ya Blue bahari yenye michirizi meupe (zinapatikana duka la shule
- Viatu vyeusi vya ngozi vyenye kamba na visigino vifupi
- Sweta rangi ya kijani jeshi.
- Soksi ndefu nyeupe (stoking) jozi mbili au zaidi
- T-shirt ya shule yenye nembo ya shule utaikuta shuleni.
- Pulneck nyeupe 2 mikono mirefu

**IWAPO MWANAO NI MWISLAMU NA ANAPENDA KUVAA KIISLAMU SARE ZA SHULE ITAKUWA NI**

- Suruali mbili (2) zisizobana rangi ya draft
- "short" kanzu mbili nyeupe urefu ni inchi kumi na mbili kutoka magotini kwenda chini, pana isiyo na mipasuo pembeni
- Hijabu (kijuba) mbili (2) vitambaa vya kufunika kichwa na mabega nyeupe visivyo na marembo yoyote
- Pulneck nyeupe 2 mikono mirefu.
- Mashuka mawili rangi ya pinki yanayopatikana kwenye duka la shule.



**Rangi ya sketi (draft )**

**MAVAZI YA KAZI / SHAMBA DRESS**

- Sketi mbili rangi ya dark blue
- Mabuti ya mvua rangi nyeusi au kijani jozi mbili (2)
- Mwavuli moja kwa ajili ya kujikinga na mvua kipindi cha masika
- Raba nyeupe au nyeusi (mwanafunzi haruhusiwi kuvaa ndala au yebo yebo nje ya bweni au darasani) ndala au yeboyebo ni kwa ajili ya matumizi ya kuoga tu
- T-shirt ya blue moja

**SARE ZA MICHEZO**


(i.) T- Shirt rangi ya blue.
(ii.) Traki suti rangi nyekundu na nyeusi yenye michirizi meupe mkononi.
(iii.) Raba jozi moja za michezo.
(iv.) Soksi za michezo jozi mbili.
(v.) Bukta rangi nyekundu.

N.B Mzazi/ mlezi utawajibika kumshonea mwanao sare zote kama zilivyotajwa hapo juu na mwanafunzi ajapo shuleni awe amevaa sare za shule au traki ya rangi iliyoelekezwa.

**SARE ZA SHULE (WAVULANA)**

a) Suruali mbili (2) za rangi ya kijani kijeshi zilizoshonwa vizuri zenye marinda mawili na mfuko mmoja wa nyuma usio na zipu na pindo la chini (turnup) la upana wa nchi 18 (suruali zilizobana au modo hazitaruhusiwa) na mkanda mweusi wa ngozi.
b) Mashati mawili meupe mawili (02) au zaidi ya mikono mirefu yenye mfuko mmoja. Mashati meupe ya tomato yanashauriwa zaidi.
c) Viatu vya rangi nyeusi vya **kufunga na kamba** na visiwe na visigino virefu pamoja na soksi ndefu nyeupe jozi mbili au zaidi.
d) Sweta la kijani kijeshi la mtindo wa V - shingoni mikono mirefu.
e) T-shirt ya shule yenye nembo ya shule utaikuta shuleni.
f) Mashuka mawili rangi ya blue
g) Soksi ndefu nyeusi (stoking) jozi mbili au zaidi

Scaning kitambaa cha sweta



**SARE ZA MICHEZO**

(a) Tracksuit ya rangi nyekundu na nyeusi yenye mistari meupe mkononi isiyo na maandishi, raba na soksi za blue.

(b) T- shirt rangi ya njano

(c) Raba jozi moja za michezo

(d) Soksi za michezo jozi mbili au zaidi

(e) Bukta rangi nyekundu

**MAVAZI YA KAZI / SHAMBA DRESSING**

- Suruali rangi ya dark blue
- Mabuti ya mvua rangi nyeusi au kijani jozi mbili (2)
- Mwavuli moja kwa ajili ya kujikinga na mvua kipindi cha masika
- Raba nyeupe au nyeusi (mwanafunzi haruhusiwi kuvaa ndala au yebo yebo nje ya bweni au darasani) ndala au yeboyebo ni kwa ajili ya matumizi ya kuoga tu
- T-shirt ya blue moja au zaidi

N.B Mzazi/ mlezi utawajibika kumshonea mwanao sare zote kama zilivyotajwa hapo juu na mwanafunzi ajapo shuleni awe amevaa sare za shule.

# 5. MICHANGO YA SHULE

| Na | Aina ya Mchango | Kiasi |
|---|---|---|
| 1. | Mchango wa Uendeshaji wa Shule | 65,000/= |
| 3. | Tahadhari | 5,000/= |
| 4. | Nembo | 5,000/= |
| 5. | Kitambulisho cha Shule | 5,000/= |
| | **Jumla** | **80,000/=** |

Fedha zote zilipwe kwenye akaunti namba**: 41210013565**

**Benki NMB**

**Jina la akaunti: WAZAZI SHULE YA SEKONDARI KAINAM**

N.B- Michango hiyo au pesa taslimu **haitapokelewa** shuleni

- Shuleni tutapokea pay slip tu ya benki
- Unashauriwa kabla ya kukabidhi pay slip ubakiwe na nakala yako

6. **Mahitaji mengine muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuleta shuleni ni:-**
   (i.) Rim mbili (02) za karatasi aina ya Rotatrim (A4)
   (ii.) Dictionary  na kamusi ni muhimu kwa anayechukua masomo ya lugha
   (iii.) Godoro la kulalia inchi $2\frac{1}{2}$ uje nayo
   (iv.) sanduku moja (tranka) moja tu lenye kufuli imara.
   (v.) Vyombo vya chakula (sahani ya mfupa au ya bati, bakuli, kijiko na kikombe. (vinapatikana kwenye **duka la shule**)
   (vi.) Ndoo moja ndogo yenye mfuniko kwa ajili ya matumizi binafsi ya mwanafunzi.
   (vii.) Aje na dawa ya meno, mswaki na mafuta ya kujipaka (mwanafunzi haruhusiwi kutumia vipodozi vya aina yoyote ile pamoja na mapambo).
   (viii.) Aje na saa ya mkononi kwa ajili ya kutunza muda **(saa zenye marembo pamoja na zile za simu hazikubaliki kabisa!!!).**
   (ix.) Aje na madaftari makubwa (counter books quire 3) yasiyopungua nane (8) pamoja na madaftari madogo madogo kumi (10) tu **(utapata kwenye duka la shule)**.

(x.) Aje na mkebe (mathematical set) moja (1) kwa wanaosoma geographia

(xi.) Aje na non - programmable calculator "kwa wale wanaochukua somo la jiografia".

**VIFAA VYA USAFI:**

a) EGM, HGK na HGFa: Aje na jembe, mopa, fagio (chelea) na panga.

b) HKL na HGLi: Aje na jembe ndoo ya lita 20, fagio (chelea) na mopa

**c)** EGM, HGK, HGFa, HGLi na HKL –aje na lita tano (5L) ya sabuni ya maji.

**7. MAMBO YA KUZINGATIA WAKATI WA KURIPOTI.**

**Wakati wa usajili mwanafunzi anatakiwa kuwa na nyaraka zifuatazo kwa ajili ya uthibitisho:-**

a) Sare ya shule ya darasani (full school uniform)

b) Barua yake ya maagizo (joining instruction)

c) Leaving certificate ya kidato cha nne/slip result -kivuli

d) Barua ya mzazi/mlezi ya kukubali nafasi hii ikiwa imejazwa kikamilifu. (**Kiambatisho B).**

e) "Medical Examination form" ambayo imejazwa vizuri na mganga wa hospitali ya serikali na siyo hospitali binafsi (Kiambatisho C).

f) Maelezo binafsi ya mzazi/mlezi kuhusu historia ya mwanafunzi pamoja na mkataba wa kutoshiriki katika mgomo, fujo na makosa ya jinai utakaojazwa na mwanafunzi pamoja na mzazi/mlezi.

8. **ONYO NA MAZINGATIO!!**

(i.) Mwanafunzi **haruhusiwi kusuka**

(ii.) Mwanafunzi haruhusiwi kuja na nguo za nyumbani.

(iii.) Mwanafunzi haruhusiwi kwenda bwenini kabla ya kukamilisha usajili wake

(iv.) Mwanafunzi **haruhusiwi kuwa na simu ya mkononi au kitu chochote kinachohusiana na simu**, iwapo atakamatwa na simu au kifaa chochote cha Simu atanyang'anywa na **KUFUKUZWA** shule **(hatarejeshewa simu au vifaa hivyo).**

(v.) Mwanafunzi haruhusiwi kuja na chakula cha aina yoyote ile shuleni

(vi.) Mwanafunzi haruhusiwi kuwa na pasi, heater, kibatari, karabai, mishumaa, radio, camera, television, jiko lolote la kupikia na sufuria.

(vii.) Mwanafunzi hatakiwi kuchelewa shule kwa tarehe iliyopangwa na iwapo atachelewa kwa muda wa siku kumi na nne (14) baada ya tarehe ya mwisho ya kuripoti bila taarifa ya maandishi atakuwa amepoteza nafasi yake.

(viii.) Mwanafunzi haruhusiwi kufuga kucha, kuweka kucha za bandia, kope za bandia, kupaka rangi kwenye kucha, lipstick, kupaka wanja, kuweka dawa kwenye nywele, kutumia vipodozi na kutumia manukato, haruhusiwi kufuga nywele. Hivyo atatakiwa kunyoa nywele zake na ziwe fupi muda wote. Haruhusiwi kunyoa kipara wala panki.

(ix.) Atatakiwa kuheshimu viongozi, wazazi/walezi, wafanyakazi wote na jamii kwa ujumla.

(x.) Atatakiwa kuhudhuria vizuri shughuli zote za ndani na nje ya darasa au ya shule.

(xi.) Atatakiwa kutekeleza kwa makini na kwa uaminifu na uadilifu mkubwa shughuli zote za shule za jioni kama ilivyo kwenye ratiba.

(xii.) Atatakiwa kuwahi katika kila shughuli za shule na nyingine atakazopangiwa

(xiii.) Atatakiwa kukimbia mara aitwapo na mtu anayemzidi umri.

(xiv.) Atatakiwa kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelezo yote juu ya kuwepo ndani au nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wake katika shule hii

(xv.) Atatakiwa kutunza usafi wa **mwili** na **mavazi** pamoja na **mazingira** yote ya shule.

(xvi.) Atatakiwa kuvaa sare ya shule iliyo ndefu na safi wakati wote anapokuwa ndani au nje ya mipaka ya shule.

(xvii.) Atatakiwa kuzingatia ratiba ya shule wakati wote.

(xviii.) Mwanafunzi anatakiwa:- kusoma, kuelewa , kuzishika na kuzifuata sheria za shule ambazo atafafanuliwa kwa kina mara tu afikapo shuleni kwani maonyo na mazingatio hayo yaliyotajwa ni baadhi tu kati ya sheria na taratibu zilizopo na zinazotakiwa kufuatwa.

**Muhimu:-** Ni vyema mwanafunzi kusindikizwa na mzazi/mlezi wake ili mzazi au mlezi huyo afahamu mazingira ya shule na mahali shule ilipo na vilevile kufahamiana na uongozi wa shule na kuwa na uhakika ya kuwa mtoto wake amefika salama mahali panapostahili.

## 9. SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE HII

shule inaendeshwa kwa mjibu wa sheria ya elimu na 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyorekebishwa kwa sheria na 10 ya mwaka 1995. Aidha inazingatia miongozo yote inayotolewa na wizara ya elimu sayansi na

teknolojia, yenye dhamana ya elimu nchini na ofisi ya Waziri mkuu-Tamisemi yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji elimu. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yatafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni.

MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA

a) Heshima kwa viongozi, wazazi , wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima
b) Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya eneo la shule kulingana na ratiba ya shule ni ya lazima
c) Kushiiriki kwa makini kufanya maandalio ya jioni(night preparation)
d) Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyingine utakazopewa
e) Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii
f) Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira
g) Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa na
h) Kutunza mali ya umma
i) Kusoma kwa bidii zote na kuhakikisha unafaulu vizuri mitihani
j) Kuongea lugha ya kiingereza kwani ndiyo lugha kuu ya mawasiliano

10. **MAMBO /MAKOSA YANAYOWEZA KUSABABISHA MWANAFUNZI KUFUKUZWA SHULE.**

(i.) Wizi
(ii.) Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa /utoro
(iii.) Kugoma na kuhamasisha mgomo
(iv.) Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla.
(v.) Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule.
(vi.) Kusuka nywele, wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni.
(vii.) Kufuga ndevu
(viii.) Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya madawa ya kulevya
(ix.) Uvutaji wa sigara.

(x.) Uasherati, uhusiano wa jinsia moja, kuoa au kuolewa.
(xi.) Kupata ujauzito au kutoa mimba
(xii.) Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi;
(xiii.) Kusababisha mimba au kumpa mimba msichana
(xiv.) Kutembelea majumba ya starehe na nyumba za kulala wageni
(xv.) Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule
(xvi.) Kudharau bendera ya Taifa
(xvii.) Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu n.k.
(xviii.) Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.

Aidha shule hii inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya Elimu Na**. 25 ya mwaka 1978** na marekebisho yake **Na. 10 ya mwaka 1995**, vile vile shule inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara yenye dhamana ya Elimu nchini.

# Fomu Na. 1

# AHADI YA MZAZI / MLEZI

Mimi______________________wa S.L.P______Mji__________Simu _____________ Ambaye kazi yangu ni ______________natamka hapa kama mzazi / mlezi wa ___________________. Ninakubali kwa hiari yangu mwanangu asome katika Shule ya Sekondari Kainam kuanzia tarehe _________________. Ninaahidi kama ifuatavyo:-

1. Kwamba nimekubali chaguo alilopewa mwanangu na sitamruhusu kubadilisha hadi apate kibali cha maandishi kutoka kwa mamlaka husika.

2. Ninaahidi kumpatia mwanangu vifaa vyote kama vilivyoainishwa katika fomu ya kujiunga ikiwemo SARE KAMILI ya shule bila kuharibu chochote.

3. Ninatambua ya kuwa walimu wanahitaji ushirikiano wangu katika kumpatia mwanangu elimu na nitashirikiana nao bega kwa bega kwa masuala yanayomuhusu mwanangu kitaaluma na nidhamu ili aweze kufikia malengo yake na ya Taifa.

4. Naahidi kuwa endapo mwanangu ataenda kinyume na taratibu zilizoainishwa katika fomu hii achukuliwe hatua stahili za kinidhamu kama alivyoorodheshewa.

Jina:__________________________ saini_________________

Tarehe:______________ Uhusiano na mwanafunzi:____________

**MEDICAL EXAMINATION FORM**

To be completed by Medical Officer from a known Public Hospital or Health Centre in respect to all entrants

Full name……………………..................Age……...Sex………..year…..

1. Blood count (Red and White) ……………………………………...
2. Urinalysis Test ……………………………………………………….
3. Syphilis test…………………………………………………………
4. T.B…………………………………………………………………
5. Eye Test ……………………………………………………………
6. Ears…………………………………………………………………
7. Spleen………………………………………………………………
8. Abdomen ……………………………………………………………….

ADDITIONAL INFORMATION: e.g. Physical impairment, family disease, chronic infections etc.

……………………………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………………………

………………………………

I certify that the above named individual is fit to pursue studies as stated above

……………………………….. ………………………………….

Name and Designation Signature and Official stamp

……………………………….. ……………………………

STATION DATE

**NOTE:**

1. Medical officer during the course of this Examination please attend the individual according to any diagnosed case.

2. The dully filled form must be handed to the Head of the School during registration week, under No circumstances should a student be registered without certification of his/her physical fitness.

# Fomu Na. 2

# AHADI YA MWANAFUNZI

Mimi mwanafunzi ________________________________Wa kidato cha Tano

chaguo______________(tahasusi) mwaka wa masomo 2024. Ninakiri

kusoma, kuelewa na kuahidi kutii taratibu zote zilizoainishwa katika fomu

iliyotumwa kwangu na Mkuu wa shule ya Sekondari Kainam.

Nitatoa ushirikiano wa kutosha kwa walimu wangu na shule kwa ujumla

katika muda wangu wote nitakaokuwa shuleni, ili niweze kupata elimu na

kuendeleza jamii na Taifa langu.

Jina:_____________________________ Saini_______________

Tarehe: ___________________

Mwisho Kwa niaba ya jumuiya ya Kainam sekondari napenda kukukaribisha Sana hapa shuleni na kukutakia safari njema na mafanikio mema katika masomo yako ya kidato cha tano na sita. "May the lord grants and bless you abundantly"

……………………..

Jina la Mkuu wa Shule……………………

MKUU WA SHULE

0782625696/0621-556407

KAINAM HIGH SCHOOL

**VITABU**

**KISWAHILI 01**

1) Taasisi ya elimu Tanzania (TET) toleo jipya (2021)
2) Sarufi maumbo ya kiswahili sanifu (SAMAKISA) (Y.M Kihore, D.p.B Massamba)
3) Sarufi miundo ya Kiswahili sanifu (SAMAKISA) (Y.M Kihore, D.p.B Massamba)
4) Nadharia ya lugha kidato cha 5 na 6 ( Nyambari Nyangine

**KISWAHILI 02**

Orodha ya vitabu teule kidato cha tano na sita

1) Taasisi ya elimu Tanzania (TET) toleo jipya (2021)

2) Orodha ya vitabu vya **riwaya**
    a) Dunia uwanja wa fujo
    b) Ua la faraja
    c) Mirathi ya hatari
    d) Wasifu wa siti Binti Saad
    e) Vuta nikuvute
    f) Asali chungu
    g) Mwana wa yungi hulewa
    h) Vipuli vya vigo
3) Vitabu vya **tamthiliya**
    a) Mukwava wa uhele
    b) Shujaa mirambo
    c) Usaliti mjini
    d) Kaptula la max
    e) Nyerere na safari ya kanaani
    f) Morani
4) Viabu vya **ushairi**
    a) Fumbo linaloelea
    b) Malenga wa ziwa kuu
    c) Andamo, msafiri safarini
    d) Wosia wa baba
    e) Dhifa
    f) Utenzi majumuiwa karne ya 21
    g) Malenga wa bara
    h) Fungate ya uhuru

**GEOGRAPHY**

**PRACTICAL GEOGRAPHY BOOKS**

1) Practical geography for advanced secondary school students book (TIE)
2) Practical geography by (Zisti kamili)
   New edition
3) Practical geography by (Haruna Masenza)
4) Practical geography in concise by (Mohamed A. (2023) (shacksy)

**PHYSICAL GEOGRAPHY BOOKS**

1) Physical geography for advanced secondary school students book form five and form six(TIE)
2) Physical geography by (D.T.Msabila)
3) Physical geography in concise by (A Kh. Mohamed (shacksy) (2023)
4) Physical geography by (Haruna Masenza)
5) Physical geography (Zisti Kamili) New Edition

Human economic geography

1) Human geography (TIE)
2) Human geography (Zisti Kamili) new edition

English language 01

1) Tanzania institute of education (TIE)
2) Nicholors Ashley advanced English
3) Nyambari nyangwine
4) Mgonja fransis

**ENGLISH LANGUAGE**

1) Advanced level literature

Reading **–novels**

- Animal farm
- Chasing the leopard finding
- The opportunistic elite
- The horizon unveiled
- Arrow of God
- A man of the people
- A giant of wheat
- Petals of blood
- No longer at ease
- Joy comes in the morning
- The lion of Yola

**Play**

- The government inspector
- An enemy of the people
- A taste of heaven

- Betrayal in the city
- I will marry when I want
- Julius casar
- Man of Kafia

**Poetry**

- Summons: poems from Tanzania
- Poets of Africa: lament of the silent and other poems
- Poets of Africa 7; boundless voices poem from Kenya
- The bleeding hearts and other poems

**HISTORY**

1) Essentials in advanced level history paper 1&2 by Salehe Yassin
2) Contemporary historical events paper 1&2 by Shibitali Tumaini
3) History for advanced secondary schools form v&vi by TIE
4) Advanced learning world history by Idrisa Msuya book 1&2
5) Medieval ages paper 2 by MMavunde
6) Zisti Kamili history paper 1 and 2 new edition (2023)

**ECONOMICS**

**ECONOMIC 01**

- Ambros Othiambo advanced economic one
- Mganda economic one
- Ambilikile advanced economic paper one
- Tanzania institute of education (TIE) advanced economic paper 2

Economic 02

- Ambros Othiambo advanced economic one
- Mganda economic 02
- Ambilikile advanced economic paper 2
- Tanzania institute of education (TIE) advanced economic paper 2

Mathematics

1) Pure mathematic chand

2) Mayombya advance mathematics form five and six
3) Tanzania institute of education (TIE) advanced mathematics

- **Historia ya Tanzania na maadili kidato cha tano na sita**
- **Academic communication advanced level form five and six**